| 8 copies

## MWONGOZO MTIHANI WA PAMOJA KISII-MARANDA

## KISWAHILI INSHA-karatasi ya kwanza(102/1

## MASWALI

1. **Umesoma tangazo katika gazeti la Mzalendo kuhusu nafasi ya kazi ya Udaktari katika hospitali kuu kwenye kaunti yako. Andika barua ya kuomba kazi hiyo na uiambatanishe na tawasifu-kazi yako.**

-Hi ni **barua Rasmi** ya kuomba ajira ya udaktari

-sura ya barua lazima iwe ifuatavyo:

i) Anwani mbili ziwepo ya mwandishi na anayeandikiwa.

Anwani ziwe wima:

Mtajo;Kwa Bwana/bibi,

MADA/KIINI/KUH kwa mfano KUH:KAZI YA UDAKTARI

ii)_Utangulizi-uwe wa moja kwa moja bila salamu

iii) Mwili-Maudhui

a) Tangazo alilipataje?gazeti lipi?Tarehe n.k.
b) Maelezo ya kibinafsi-uraia,mahali pa kuzaliwa, n.k.
c) Masomo/kiwango cha elimu kuanzia chekechea,msingi,upili na chuo kikuu.ufanisi katika vyango hivi vyote vya elimu.

'2

d) Tajiriba au ujuzi wa kazi hiyo na ufanisi tangu upate kazi inayohusiana na udaktari pengine uliyokuwa ukifanya ilikuwa ya kujitolea tu.

iv) Hitimisho-sahihi na jina la mwandishi

TAWASIFU-KAZI

I) Kichwa kiwe na neno Tawasifu-kazi

II) Habari ya maelezo ya kibinafsi k.m

Jina rasmi.............................................

Tarehe ya kuzaliwa.................................

Mahali pa kuzaliwa.................................

Jinsia.....................................................

Umri......................................................

Lugha.....................................................

Dini.......................................................

Anwani...................................................

Nambari ya kitambulisho....................

Barua pepe.........................................

Nambari ya simu..................................

iii) Elimu

Kuanzia kiwango cha juu hadi cha chini

Katika upande wa kushoto mwaka au wakati uandikwe ukiambatanishwa na viwango vya elimu

iv) Tajiriba

a) Maelezo ya tajiriba ya kazi hii
b) Anaweza kuonyesha tajiriba nyinginezo

v) Uraibu k.m kusakata ngoma, kusoma n.k

vii) Uanachama k.m Chama cha Mazingira

viii) Wadhamini/Warejelewa-Mtahiniwa aonyeshe angalau wawili . majina yao , vyeo vyao,anwani na nambari zao za simu/barua pepe.

**2. Nchini Kenya michezo ya kamari imeharibu vijana wengi sana na inastahili kupigwa marufuku. Jadili.**

**Michezo ya kamari imeleta faida kwa vijana kwa njia zifuatazo:-**

i) Huleta ajira kwa vijana katika mashirika hayo ya kamari

ii) Serikali hupata ushuru

iii) Njia ya kujitajirisha kwa haraka

iv) Ni aina ya burudani inapotoka katika televisheni na Redio

v) Kampuni hizi huweza kufadhili michezo na elimu

vi) Husaidia kupitisha wakati

vii) Husaidia katika kuinua jamii au kuzalisha mali kwa mfano mshindi atawapa wengne ajira.

**Michezo ya kamari imeharibu vijana kwa njia zifuatazo:-**

i) Huchangia utovu wa nidhamu kwa mfano wizi ili wapate pesa za kushiriki katika michezo.

ii) Kufilisisha jamii kwa sababu ya utegemezi.

iii) Washiriki kutopanwa mawazo yao ya jinsi ya kupata riziki

iv) Ni njia ya kuvunja sheria

v) Kupotosha jamii kwa mfano washiriki hutumia pesa kwa mfano za kulipa karo na matumizi mengine kuucheza mchezo wa kamari.

vi) Huchangia wanafunzi kuacha shule.

vii) Kuruhusu watu wa umri mdogo kushiriki

viii) Huwafanya vijana kuwa wavivu.

Lazima ashughulikie pande zote mbili za swali na akishughuikia upande mmoja tu asipite alama 10.

**3. Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali :Mwenye pupa hadiriki kula tamu**

-Afanyaye mambo kwa pupa au kwa haraka bila uangalifu hupata madhara.

-kisa kiguzie pande mbili za methali; kwanza kionyeshe hali ya kutokuwa na subira na pili, kionyeshe athari za kukosa subira .

-maana si muhimu mradi tu atunge kisa amb acho ni kimoja tu.

-lazima ashughulikie pande zote mbili za methali na akizingatia upande mmoja asipite alama 10

-lazima awe na kichwa ambacho ni methali yenyewe na akikosa aadhibiwe kimtindo.

**4. Andika insha itakayomalizia kwa maneno haya.**

...tangu siku hiyo sijawahi kuuasi ushauri wa wakuu.

i) Mtahiniwa atunge kisa kinachoashiria aliyeenda kinyume cha ushauri au wosia au mawaidha aliyopewa akadhurika

ii) Lazima awe na kichwa na bila kichwa ataadhibiwa kimtindo